# Kanuni za Uadilifu na kanuni za maadili mema









# Yaliyomo


MANENO YA UTANGULIZI KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI 3

KANUNI ZA MAADILI NA AHADI ZA LIMAGRAIN 4

A. Kuheshimu jumuiya ya wakulima wake na wadau wake 5
B. Kuheshimu wafanyakazi wake 6
C. Kutunza mazingira 7
D. Kutekeleza kanuni za sheria ya ushindani 8
E. Kujitahidi kuwaridhisha wateja na watumiaji wake 8
F. Kuimarisha uhusiano wenye usawa na haki kwa wasambazaji na washirika 9
G. Kufuata tabia husika kulingana na nchi na maeneo ambako Limagrain ipo 9

KAMATI TENDAJI YA LIMAGRAIN' IMEJITOLEA KUPAMBANA NA UFISADI 10

MAADILI NA TABIA ZA WANAUME NA WANAWAKE HAPA LIMAGRAIN 12

1. Kulinda taswira na sifa nzuri za Limagrain 13
2. Kuheshimu na kulinda rasilimali 14
3. Kuwa muadilifu na kuepuka migongano ya maslahi 15
4. Kuzuia usambazaji wa taarifa zisizo za umma za kifedha na biashara za ndani 16
5. Kuhakikisha ulinzi wa haki miliki 17

KUHOJI KAMA MSUKUMO WA MAADILI YETU 18

Nani wa kuwasiliana naye kwa swali au tatizo lolote

MFUMO WA KUTOA TAARIFA 19

Wajibu wa kila mfanyakazi wa Limagrain

MADHARA YA KUTOTII KANUNI ZA MAADILI MEMA 21

FAHARASA 24


Toleo lilisasishwa Mei 2022 2022

# MANENO YA UTANGULIZI KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI

Katika mwaka wa 2015, Limagrain ilianza kutumia Kanuni yake ya kwanza ya Maadili Mema ili kushughulikia changamoto kwa misingi ya sera ya jumla: kuimarisha kanuni za maadili ya biashara yetu kwa kufuata taratibu za sasa, na hivyo basi kufungamanisha shughuli zake na msukumo wa uendelevu na uwajinikaji husika kwa ajili ya maendeleo.

Kwa kweli, shughuli zetu, ziwe zinahusu utafiti, uzalishaji au masoko ya mbegu na bidhaa za vyakula zinazotokana na kilimo, zipo kwenye kitovu cha changamoto za kijamii, ushirika na mazingira ambayo yanaongezeka kuwa ngumu na iliyodhibitiwa. Wateja wetu, iwapo ni kampuni au watumiaji, pia wana masharti mengi ukilinganisha na uwezo wetu wa kjumuisha ushughulikiaji wa changamoto hizi zote.

Limagrain inajitoka katika masoko ya kitaifa na kimataifa ambayo yanabadilika haraka. Haya ni masoko ambako kuna kanuni za kisheria na, hivyo basi kwa kiwango kikubwa, masharti yameundwa kutoka kwenye kanuni za msingi, mikataba na viwango.

Toleo hili jipya la Kanuni za Uadilifu na Kanuni za Maadili Mema linazingatia mabadaliko ya hivi karibuni ya kisheria na ni sehemu ya mpango wetu wa Wajibu wa Pamoja wa Kijamii (CSR), na kwa kawaida imejikita kwenye utamaduni wetu wa ushirika na maadili yetu ya maendeleo, uvumilivu na ushirikiano. Huu ni mwongozo wa kudumisha uangalifu wetu, mfumo unaofafanua msingi mzuri, zana ya kumuhimiza kila mmoja kufikiria kuhusu changamoto hizi, dira ya kutuonyesha muelekeo wa shuluhisho.

Hakuna mfanya kazi, kutoka kampuni au nchi yoyote anayofanyia kazi ambaye anaweza kudai kwamba anafanya kwa maslahi ya Limagrain, iwapo anafanya kinyume cha maadili au sheria na kanuni za Limagrain zilizoorodheshwa katika hati hii.

Kanuni hizi za Uadilifu na Kanuni hizi za Maadili Mema zinaashiria ahadi yetu ya pamoja ya kwa maendeleo endelevu na yenye uwajibikaji wa shughuli zetu duniani kote. Kwa hivyo, ninatarajia kwamba sisi sote tutazifahamu kanuni na kuzirejelea katika kazi yetu hapa Limagrain.



**Sébastien Chauffaut**



# KANUNI ZA UADILIFU NA AHADI ZA LIMAGRAIN



## A. Kuheshimu jumuiya ya wakulima wake na wadau wake

Limagrain ina nia ya kulasimisha kanuni za uadilifu na ahadi ambazo zitatumika kwa wadau wake wakuu: jumuiya ya wakulima, wanahisa, wafanyakazi, wasambazaji, washirika na wawakilishi katika nchi ambako Limagrain ipo. Ahadi za Limagrain zimeunganishwa na za washirika wake, ambao ni mabalozi wao wa kila siku.

Limagrain ni kundi la ushirika la kimataifa, na hisa inajumuisha wakulima ambao ni washirika wa Coopérative Limagrain. Wanahisa wadogo wa nje wanaimarisha mshikamano wa taasisi hii na wanachangia maendeleo ya muda mrefu wa Kundi la Kampuni.

Limagrain inahakikisha kwamba matarajio ya wanahisa wake wote wanakubaliana na kuzingatia, kanuni za soko la hisa zilizotafsiriwa na Mamlaka ya Soko la Fedha (AMF) zinatumika, na kwamba kanuni za utawala bora zinatumika.

Pamoja na haya, Limagrain inafuata mapendekezo yaliyowekwa na MiddleNext, faharisi ya maadili ya soko la hisa kwa ajili ya mtaji wa kati, ambayo inaelezea utendaji sahihi wa aina hii ya kampuni.

Limagrain huwapa wanahisa wake taarifa za ziada na sahihi, kulingana na kanuni zinazotumika, mara zote au wakati wowote zinapohalalishwa.

# B. Kuheshimu wafanyakazi wake

## HAKIKISHO LA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI

Limagrain inazingatia kuwa jukumu lake kuu kwa jamii ni kuwapa wafanyakazi wake na wafanyakazi wote wasio wa Limagrain wanaofanya kazi kwenye maeneo ya Kundi la Kampuni mazingira ambayo yanalinda afya zao na usalama wao vilevile mazingira ya kazi yenye ubora wa juu.

Kwa dhumuni hili, Limagrain imedhamiria kufuata utekelezaji wa sheria wa kila nchi vilevile kanuni na viwango vya ndani ambavyo vinatumika kwa misingi ya usafi, afya na usalama. Limagrain imedhamiria kuweka viwango vya mfumo wa kumbukumbu kuhusiana na masuala ya afya na usalama.

## KUWAHESHIMU WATU NA MAISHA YAO BINAFSI

Limagrain imejidhatiti kuwatendea haki na kwa mtazamo unaofaa, kuheshimu utu wao na utimilifu wao wa kimwili na nafsi.

Wafanyakazi wa Limagrain huajiriwa bila ubaguzi wa misingi ya jinsia, umri, utaifa, dini, muelekeo wa kingono, mwonekano wa kimwili, hali ya afya, ulemavu, uanachama wa chama cha wafanyakazi au maoni ya kisiasa.

Pia Limagrain inaheshimu maisha binafsi ya wafanyakazi wake na haiingilii shughuli zao nje ya kazi. Inadumisha msimamo usioegemea upande wowote kuhusiana na maoni ya kisiasa na kifalsafa au imani ya kidini, na inakataza mahubiri mahali pa kazi.

Zaidi ya hiyo, Limagrain inataka maendeleo binafsi na ya kitaalam kwa wafanyakazi wake.

Limagrain inajitahidi kutoa fursa sawa ya kupata mafunzo ya kitaalam kwa wote ili wafanyakazi wote waweze kudumisha na kuendeleza ujuzi wao.

Limagrain inajitolea kwa mijadala ya kijamii na inaifanya kwa ukweli na uaminifu.




## KULINDA DATA ZA MTU BINAFSI

Kulinda data za mtu binafsi ni eneo mahususi la kutiliwa mkazo. Data za asili ya kibinafsi za wateja, washirika wa kibiashara, na wafanyakazi wetu hazipaswi kukusanywa, kurekodiwa, kuchakatwa, au kutumwa, isipokuwa ndani ya mawanda ya sheria mahsusi za nchi.

Limagrain imedhamiria kukusanya na kuchakata data za kibinafsi za jumuiya yake ya wakulima, wafanyakazi na watu wengine, matumizi yaliyokusudiwa na halali tu ambayo yanahusiana na dhumuni la shughuli za uchakataji.

Taarifa stahiki na muhimu zitachukuliwa kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

Kwa mfano, taarifa zinazotumika kwa ajili ya uchakataji wa kompyuta za orodha ya wapokea mshahara zinazohusu utambulisho, hali ya familia, maisha ya kitaalam na vipengele vya ujira wa mfanyakazi. Haziwezi kutumika kwa madhumuni mengine.

Aidha, kuhusiana na kulinda taarifa za mtu binafsi, Limagrain inaahidi kufuata sheria za nchi ambazo inaendesha shughuli zake, kama vile kanuni za ukomo wa muda wa kuhifadhi taarifa, na haki ya kupata, ushauri, idhini, masahihisho, taarifa, ubebekaji, ufutaji, au upinzani.

Limagrain inatoa hakikisho la usalama, faragha na uadilifu wa data za mtu binafsi za wafanyakazi wake na watu wengine.

# C. Kutunza mazingira

Limagrain pia inaahidi kutoa mchango mkubwa wa kuheshimu mazingira kwa matumizi ya utunzaji wa rasilimali ambazo zimeunganishwa na uboreshaji wa michakato ya uzalishaji katika nyenzo zake duniani kote.

Limagrain imeanza kutumia mkakati wa kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa mazingira (EMS) na kuboresha shughuli zake ili kutunza maliasili, kulinda mazingira, na kuendana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Katika soko la mbegu, Limagrain inajitahidi kuunda jamii zilizotengenezwa kuendana na utofauti wa mazingira na kueneza shughuli nzuri na husika za kilimo kwa jumuiya ya wakulima na washirika wake. Katika soko la chakula cha kilimo, Limagrain inajitahidi kukuza na kutekeleza viwango bora zaidi na kanuni za viwandani ambazo zinatekeleza sheria za Ulaya na kimataifa.



## D. Kutekeleza kanuni ya sheria ya ushindani

Limagrain inaahidi kutekeleza mikataba ya kisheria na Udhibiti, ya kitaifa na kimataifa inayohusiana na kanuni za sheria ya ushindani. Dhumuni la kanuni hizi ni kutoa hakikisho la ushindani huru kwenye soko.

Kwa kufuata kanuni hizi, sera ya Limagrain ni kuzuia aina yoyote ya mjadala au mawasiliano na washindani kuhusu bei, vyanzo na mgawanyo wa masoko na wateja.

Limagrain pia inakataza matendo mabaya pale kampuni inatawala katika soko husika. Hali kadhalika, Limagrain imejidhatiti kupata uthibitisho kutoka mamlaka mbalimbali wakati wa miamala ya pamoja au ushirika ambayo una athari kwenye soko, ndani ya mfumo wa sheria husika.

Limagrain inahakikisha kwamba wafanyakazi wote wanajulishwa kwamba ukiukaji wowote wa hatua hizi unaweza kuhusisha dhima ya Limagrain vilevile dhima yao binafsi.

## E. Kujitahidi kuwalidhisha wateja na watumiaji wake

Kwa kuwa inatambulika katika masoko yake yote kwa ubora wa bidhaa zake, Limagrain inaguswa na mahitaji na matarajio ya watumiaji na wateja wake.



Limagrain inadhibiti, inatathmini na kuboresha bidhaa na huduma zake ili kuhakikisha ubora na usalama katika kila hatua za michakato yake ya uundaji, uzalishaji na usambazaji.

Limagrain imejidhatiti kutumia viwango vya hali ya juu vya mawasiliano, kuheshimu masharti ya eneo husika kuhusiana na vitu na njia iliyotumika kuwajulisha wateja na watumiaji.

Limagrain inahakikisha kwamba taarifa zote zinazotolewa ni mpya, sahihi, hazina upendeleo na zinatumainiwa, na kwamba zimekamilika ipasavyo kuelewa ubora wa bidhaa na jinsi inavyopaswa kutumika.

## F. Kuimarisha uhusiano wenye usawa na haki kwa wasambazaji wake

Limagrain inachagua wauzaji na wakandarasi wadogo wake kulingana na vigezo vya malengo na inahakikisha kwamba mahusiano yake ya kibiashara na ya kimkataba yanawiana kadri muda unavyoenda.

Wauzaji na wakandarasi wadogo wanatakiwa kufuata masharti ya kisheria na utendaji wao lazima upimike bila upendeleo.

Limagrain wapo makini sana kutoingia mkataba na wauzaji ambao wanatumia wafanyakazi watoto au kuwafanyisha kazi watu kwa lazima.

Limagrain wako makini kuhakikisha washirika wao wanaheshimu masharti ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani kuhusu haki za msingi za jamii.



## G. Kufuata tabia husika kulingana na nchi na maeneo ambako Limagrain ipo

Katika maendeleo yake ya kijografia, Limagrain inajitahidi kuchukua maadili husika kwa kuzingatia nchi zote ambako Kundi la Kampuni linaendesha shughuli zake.

Limagrain inahaikisha kwamba kampuni zake tanzu zinafuata sheria na masharti ambayo yanatumika katika kila nchi ambayo wanatoka.

Hasa, Limagrain inahakikisha kwamba maendeleo yake yanaheshimu mazingira asilia na tamaduni za ukanda ambao wapo.

Kutokana na shughuli zake, Limagrain inashiriki katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii ambazo Limagrain ipo, na jambo mahususi kwa ajili ya maendeleo ya muda mrefu.

Limagrain inajizuia kutoa ahadi zozote au kutoa msaada wa aina yoyote kwa namna yoyote kwa chama cha siasa au kikundi cha kidini.

# Kamati Tendaji ya Limag
# imejitolea kupambana n

Kwa nini kupambana na ufisadi lazima iwe kipaumbele?
“Sio tatizo baya sana!”, “Mara zote tumefanya hivyo!”, “Ni njia pekee ya kupeleka mbele faili!”, “Hapa, hakuna njia nyingine!”
Huu ni baadhi ya ushughulikiaji wa kawaida tuliousikia pale suala la ufisadi linapoletwa pamoja na dhamira ya kupambana na matendo kama hayo.

**Hivyo, kwa nini tujaribu kuibadilisha?**

> Kwa sababu ya nia ya kutekeleza sheria ya kupinga ufisadi?

Bila shaka. Serikali nyingi zina sheria mahususi zinazotumika. Baadhi [(1)] ya sheria hizi zinatumika katika nchi zilizo nje ya mipaka ya nchi mahususi. Sheria kali na kandamizi zaidi zinapatikana nchini Uingereza, Marekani, Canada, na Ufaransa. Sheria hizi hazitumiki tu katika matendo yanayofanywa nje ya mipaka asili ya kitaifa, lakini pia zinaweza kubeba hukumu za kwenda jela au kulipa faini ambazo zinaweza kufikia makumi au mamia ya mamilioni ya euro. Sheria hizi zinatumika katika shirika letu kwa wale wote wanaofanyaka kazi nasi. Sharti tuziheshimu na lazima tuzifuate.

> Kwa sababu ya uaminifu wa washirika wengine kwenye soko

Hakuna shaka. Ufisadi unaharibu mwenendo wa soko kwa kupotosha ushindani. Lakini si bora zaidi kuchaguliwa na wateja na washirika wetu wa kibiashara kwa ubora wa bidhaa na huduma zetu pekee badala ya kuegemea kwenye matendo yasiyo ya uaminifu?

[(1)] Orodha kamili ya nchi ambazo kufikia Machi 2022 zilikuwa na sheria za kukabiliana na ufisadi zinazotumika nchini na katika nchi nyingine; Ajentina, Australia, Ubelgiji, Brazili, Canada, Uchina, Ufaransa, Ujerumani, India, Meksiko, Nikaragua, Urusi, Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Uingereza, Marekani

# grain'
# a ufisadi.

Kwanza kabisa, ufisadi ni kizingiti kikuu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii duniani kote!

Kila mwaka, zaidi ya dola USD bilioni 1,000 zinalipwa kama hongo na Dola USD bilioni 2,600 zinapotea kutokana na ubadhirifu, hii ni 5% ya Pato la Kitaifa duniani kote, karibu mara mbili ya Pato la Kitaifa la Ufaransa. Lakini ufisadi, ni thamani kubwa ya mapato yanayotokana na ushuru wa nchi yanayopotea, hauwezi kufikiriwa tu kwa misingi ya pesa. Kampuni ambazo zinalipa rushwa zinarudisha nyuma uadilifu wa nchi ambazo zinaendesha shughuli zao, hivyo kuongeza matatizo ya umasikini na uongozi. Ufisadi unapunguza ufanisi na ubora wa huduma za umma. Zinawaweka watu walio katika mazingira magumu katika hali hiyo ya umaskini uliokithiri, zinaongeza kutokuwepo kwa usawa, na kuongeza hali ya udhaifu.

Matatizo haya huathiri jamii nzima, kwa kuwa ukuaji wa uchumi unawezeshwa na ukuaji wa rasilimali watu, yaani, watu walioelimika wenye afya njema.Hata hivyo, ukuaji wa hii rasilimali watu unadumazwa na rushwa na athari yake kubwa inaweza kupimwa: kutojua kusoma na vifo vya watoto wachanga kunahusiana na rushwa katika nchi. Kama uthibitisho wa madhara ya ufisadi, hivi ndivyo António Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, alielezea katika maneno yake ya utangulizi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Ufisadi mnamo Desemba 2021: “Kubakiliana na ufisadi ni muhimu ili kulinda haki za kibinadamu na kukuza uwajibikali wa kisiasa. Ni hatua muhimu katika ujumuishaji, maendeleo endelevu.»

Kukabiliana na ufisadi kwa hivyo ni muhimu, bila kujali uwiano au mizani! Hakuna ufidiaji wowote wenye thamani ya hatua hii. Inahitajika ahadi ya kimataifa na kuweka wazi jukumu ambalo kampuni inajitahidi kupeleka katika jamii vilevile maadili ambayo inalenga kuyatumia na kuyahimiza. Limagrain inadhamiria kuchangia kwa kutovumilia kitendo chochote cha rushwa ndani ya kampuni kokote kule kinapoweza kutokea duniani kote, na Kamati Kuu ya Kundi la Kampuni, na sisi ni wajumbe wa kamati, tutaisimamia kwa matarajio makubwa.

***Limagrain inakusudia kuchangia kwa kutovumilia kitendo chochote cha ufisadi katika kampuni popote pale kitakapotokea ulimwenguni kote, na Kamati Tendaji ya Limagrain itafuatilia hili kwa azma kubwa.***



# MAADILI MEMA NA TABIA NJEMA YA WANAMUME NA WANAWAKE HAPA LIMAGRAIN



## 1. Kuhifadhi taswira na sifa nzuri za Limagrain

Swali halijumuishi kujaribu kupanga kwa ajili ya kila kitu au kuwekea kanuni kila kitu. Hata hivyo, kanuni chache bayana na madhubuti, zilizojumuishwa na wazo la uwajibikaji wa kila mtu na busara ya wote, zinaunda marejeo ya kila siku.

Taswira na sifa ya Limagrain ni vipengele muhimu katika uwezo wake wa kuendeleza na kuvutia wafanyakazi wapya. Hivyo, kila mfanyakazi ndani ya eneo lake la kazi analinda taswira na sifa nzuri ya Limagrain. Kila mmoja lazima afahamu kwamba kuchapisha maudhui ambayo yanaipaka matope Limagrain, maoni yanayowakashifu wenzako, washindani, au washirika, na kutoa taarifa za siri kuhusu Limagrain hakuruhusiwi.

Wingi wa zana za kidijiti, mitandao ya kijamii, tovuti za kusambaza taarifa, majukwaa na blogu zinafanya iwe rahisi kwa kila mmoja kujieleza, hivyo tunapaswa kuwa waangalifu.

*Ili kusaidia urasimishaji wa mipaka ambayo inapaswa kuheshimika, Miongozo kwa ajili ya kutumia mitandao ya kijamii inapatikana kwa wafanyakazi wote kwenye Intranet ya Limagrain.*

### *Tabia inayotarajiwa*

*Kila mfanyakazi lazima akumbuke kwamba:*

- *taarifa yoyote iliyowekwa kwenye mtandao anaweza kuipata mtu yeyote, mahali popote, na bila kikomo katika suala la muda;*
- *matumizi ya vyanzo vya taarifa vinapaswa kufuata maandiko ambayo yanatumia (sheria, kanuni, kanuni za maadili mema, mikataba), masharti kuhusiana na uaminifu na kanuni kwa ajili ya tahadhari, usalama na maadili mema;*
- *wafanyakazi wanaweza kuwajibishwa kwa maudhui waliyochapisha kwenye mtandao.*

# 2. Kuheshimu na kulinda rasilimali

Mali za Limagrain zinajumuisha vitu halisi kama vile vifaa, magari, kompyuta, nyenzo, vilevile mali zisizoshikika kama vile chapa, hati miliki, vyeti vya ulinzi wa jamii ya mimea, rasilimali za maumbile, maarifa na taarifa za siri.

### VITU HALISI

Kila mfanyakazi anahakikisha kwamba mali za Limagrain zinatumika vizuri na kwa namna inayopimika, kulinda uadilifu wao na kuhakikisha hasa kwamba zinatumika tu katika mfumo wa shughuli za kitaalam za kampuni na si kwa matumizi binafsi yasiyoidhinishwa.



### MALI ZISIZOSHIKIKA IKIWEMO DATA NA TAARIFA NYETI NA FARAGHA

Taarifa zozote zisizo za umma zilizoandaliwa ndani ya Limagrain, ikiwemo zile ambazo zinahusiana na rasilimali za maumbile, utafiti na maendeleo, data za uzalishaji, gharama, bei, mauzo, faida, masoko, wateja, washirika na shughuli za kibiashara zinaunda rasilimali muhimu katika mkakati wa Limagrain na haziwezi kuwekwa wazi na mfanyakazi bila kupata idhini.

Kila mfanyakazi anapaswa kuhakikisha kwamba faragha inalindwa na kwamba taarifa yoyote ya siri ambayo ni mali ya kampuni au watu wengine inalindwa na kwamba haitumiki bila idhini.

### *Tabia inayotarajiwa*

*Wafanyakazi wote lazima waheshimu faragha ya taarifa ambayo wanaifahamu ndani ya mawanda ya kazi zao.*

*Wafanyakazi wote ambao wanaingilia katika mradi wowote kwa namna yoyote, lazima wahakikishe kwamba:*

- *wanafahamu na kuheshimu masharti kuhusiana na faragha;*
- *mara zote wajitahidi kuwa waangalifu wakati wa mazungumzo katika maeneo ya umma (gari-moshi, ndege, migahawa, semina n.k.);*
- *waheshimu masharti ya kutotoa taarifa za siri kwa mdomo, kwa maandishi au kielekroniki.*

*Mfanyakazi yeyote ambaye anaondoka kwenye Kundi la Kampuni lazima akubaliane na masharti ya faragha.*

# 3. Kuwa muadilifu na kuepuka migongano ya maslahi

Wafanyakazi wote lazima wachukue mwenendo wa uadilifu katika mahusiano yao ya kitaalam.

Limagrain inajitahidi kutekeleza amri ya serikali na mikataba ya kisheria katika kupambana na rushwa na utakatishaji fedha (tazama ukurasa wa 10 “Ahadi yetu kupambana dhidi ya rushwa”), na, katika mwenendo wa uhusiano wa kibiashara na kifedha, kuzingatia mapendekezo ya taasisi za kitaifa na kimataifa kama vile OFAC kuhusu vikwazo vya kiuchumi.

Katika mfumo huu, Limagrain inatenda kuzuia aina yoyote ya rushwa au utakatishaji fedha haramu. Kanuni hii ni muhimu hasa katika mfumo wa makubaliano na wawakilishi wa vyombo vya serikali na taasisi za umma.

Wafanyakazi hawawezi kutenda wenyewe kwa njia ya kuridhisha kuhusiana na rushwa hai (kutoa rushwa) au rushwa isiyo hai (kupokea rushwa).

Limagrain inaidhinisha zawadi na ukarimu ambao unafaa na halali tu, uliotolewa ndani ya mfumo wa mahusiano yake ya kibiashara.

Ahadi yoyote inayotolewa na mfanyakazi kwa niaba ya Limagrain, ya zawadi, burudani au huduma za bila malipo inaweza kutolewa tu kama kunaendana na utekelezaji wa sasa na hakuvunji sheria yoyote ya sasa.

Vivyo hivyo kwa zawadi au ukarimu walioupata wafanyakazi wa Limagrain.

Pale shughuli binafsi, za kijamii, za kifedha, au za kisiasa za wafanyakazi zinaathiri au zinaelekea kuathiri uhalisia wao na uaminifu wao kwenye Limagrain, mgongano wa maslahi unaweza kujitokeza na unapaswa kushughulikiwa kwa usahihi.



### *Tabia inayotarajiwa*

*Kila mfanyakazi anakubali kutopokea zawadi yoyote*, burudani au upendeleo binafsi wa kiasi ambacho hakina sababu za msingi kuhusiana na sheria za forodha na kuzuia rushwa, ambayo inaelekea kuathiri maamuzi.*

*Wafanyakazi wote wakati wote lazima waepuke migongano* kati ya maslahi binafsi na yale ya Limagrain; migongano hiyo inaweza kuongezeka wakati wa makubaliano na mshirika wa kibiashara, mfanyakazi mwenzako au mtu mwingine.*

*(*) inarejelea jarida la ndani linalotumika*


# 4. Kuzuia usambazaji wa taarifa za fedha zisizo za umma na kukabiliana na biashara za ndani

Kila mfanyakazi lazima atunze siri ya taarifa zozote za ndani na zisizo za umma zinazohusu Limagrain ambazo zinaweza kuathiri bei ya soko la fedha la kampuni zake zilizoorodheshwa. Matumizi ya taarifa kama hizo, kwa madhumuni ya faida binafsi au ya mtu mwingine, hayaruhusiwi.

Kwa mujibu wa sheria za biashara za wenyeji, hairuhusiwi, ama moja kwa moja au isivyo moja kwa moja, kununua, kuuza au kubadilishana ulinzi wa kampuni iliyoorodheshwa ya Limagrain, kulingana na taarifa ambayo si kwa ajili ya matumizi ya umma.

Mkataba wa Biashara wa Wenyeji unaweza kupatikana kwenye Intranet ya Limagrain.

Kwa kwaida, Limagrain hulaani matendo yoyote ambayo yanaenda kinyume na uwazi wa soko na masharti ya soko la hisa hasa kwa kusambaza uvumi au matumizi ya taarifa za siri.




***Tabia inayotarajiwa***

*Wafanyakazi wote lazima wahakikishe kwamba wanazuia usambaaji wa taarifa za siri ndani vilevile nje, hasa kwa wale ambao wanahitaji kuzifahamu na kuchukua hatua ili kutoa hakikisho la usiri wa taarifa na kutotoa taarifa kwa watu wengine.*

*Wafanyakazi wote lazima wakumbuke kwamba wanaweza kuwajibishwa binafsi.*

# 5. Kuhakikisha ulinzi wa haki miliki




Limagrain inafikiria kwamba kulinda hati miliki zake (hati miliki, vyeti vya ulinzi wa jamii za mimea, siri za biashara, michoro & modeli, chapa, hakimiliki, programu tumizi, kanzidata au nyingine) ni muhimu kwa maendeleo yake na uthabiti wake.

Hivyo, kila mfanyakazi lazima alinde hati miliki ya Kundi la Kampuni kwa kuheshimu faragha ya haki hizi. Aidha, Limagrain inaheshimu hati miliki ya washirika na washindani.

### *Tabia inayotarajiwa*

*Kila mfanyakazi wa Limagrain lazima achukue hatua zote kuhakikisha kwamba uundaji wa Limagrain unanufaika na ulinzi mzuri kuhusiana na hati miliki, huku wakiheshimu faragha inayohusiana na haki hizi.*

*Kila mfanyakazi lazima afute masharti waliyokubaliana na Limagrain vilevile hati miliki za watu wengine ambazo zinatumika na ni halali katika kila eneo.*

*Mfanyakazi yeyote ambaye anaondoka kwenye Kundi la Kampuni lazima akubaliane na masharti yale ya faragha na kuheshimu hati miliki.*



# KUHOJI KAMA MSUKUMO WA MAADILI YETU

## Nani wa kuwasiliana naye kwa swali au tatizo lolote

Kwa maswali yoyote kuhusu ukalimani wa nyaraka hii, wafanyakazi wanaweza, ndani ya kampuni yao na kwa siri, kuwasiliana na meneja wao, meneja wa Rasilimali Watu au idara ya maswala ya sheria, na watu hawa kwa upande wao wanaweza kuwasiliana na Ngazi ya Juu ya Uongozi.

Inaweza kuonekana rahisi kubaki kimya au kuyafumbia macho, lakini ahadi ya Kundi la Kampuni inamaanisha kwamba Limagrain kamwe haiwezi kupuuzia tatizo linalohusiana na Kanuni hii. Wafanyakazi kamwe wasisite kutamatisha shughuli au utendaji ambao unaonekana kutofuata kanuni za Maadili na kuomba ushauri kama inafaa kutoka kwa watu mbalimbali wa karibu waliopo kwa ajili ya kujadili suala hilo.

**?**

**JE, KUNA MASHAKA KUHUSIANA NA SUALA HILO?**

**Jiulize mwenyewe maswali machache rahisi:**

- Je, suala unaloitilia shaka ni halali?
- Je, inafuata Kanuni za Uadilifu na Kanuni za Maadili Mema ya Limagrain?
- Je, inaiweka Limagrain kwenye hatari isiyokubalika au je, inaharibu maslahi ya Limagrain kwa muda mfupi, wa kati, au mrefu?
- Je, inafanana na ahadi za Limagrain na je, hakikisho la Limagrain limetolewa ndani au nje?
- Je, ni namna gani hali hii itatazamwa na watu wengine: meneja wako, wenzako, au familia yako?
- Je, ninaweza kulizungumzia suala hili kwa uhuru au je, nina mgogoro wa dhamiri pale ninapolifikilia?
- Je, nini kitatokea ikiwa suala hili litaripotiwa kwenye vyombo vya habari au kwenye mitandao ya kijamii?

**Swali?**
**code-of-conduct@limagrain.com**

# MFUMO WA KUTOA TAARIFA

## Wajibu wa kila mfanyakazi wa Limagrain

Mfumo wa tahadhari unapatikana kwa wenzako wote ili wajulishwe kuhusu tukio lolote ambalo linaenda kinyume na “Kanuni za Nidhamu na Kanuni za Maadili Mema.”

Wafanyakazi wote wa Limagrain, halikadhalika wafanyakazi wa muda au wa nje, au watu wengine wowote wanaoshirikiana na Limagrain, wanaweza, ndani ya mfumo wa shuguli zao za kitaalam, kushuhudia matendo ya matukio, au tabia kinyume na masharti ya Kanuni za Nidhamu na Kanuni ya Maadili Mema.

Wafanyakazi wote wana wajibu wa kuripoti matukio yoyote wanayojua haraka iwezekanavyo, kwanza kwa meneja wa kitengo chao, au ngazi ya juu ya uongozi (meneja Rasilimali Watu, Kitengo cha Biashara au Mkurugenzi Mkuu wa kampuni tanzu) kwa wafanyakazi au, watu wengine, mtu wao wa karibu kama uwezekano upo.

Wanaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Kamati ya Usimamizi wa Utoaji Taarifa ya Limagrain kwa:
**alert@limagrain.com**

Kupokea na Kuelekeza utoaji taarifa kunapaswa kufanywe kwa usiri mkubwa kwa kufuata masharti yanayofaa ya kisheria na utaratibu uliopo Limagrain.

Utekelezaji wa mfumo wa kutoa taarifa ni matumizi ya sheria ya Ufaransa Namba 2016-1691 ya Desemba 9, 2016, inayoitwa “Sapin II,” inayohusiana na uwazi, kuzuia rushwa, na usasishaji wa maisha ya kiuchumi. Pia inaongeza mfumo wa kutoa taarifa kwa kufafanua utawala wote kwa ajili ya kuwalinda watoa taarifa.
“Mfumo wa kutoa taarifa” na “ulinzi wa watoa taarifa” ni taratibu mbili zilizofafanuliwa na sheria. Kufuata masharti yake kunaamua uhalali wake.
Nchi zingine ambazo Limagrain inaendesha shughuli zake zina sheria zinazofanana.



# MADHARA YA KUTOFUATA KANUNI ZA MAADILI MEMA



Kanuni za maadili ya biashara zinalenga kuileta kampuni kwenye utiifu wa sheria mbalimbali za kimataifa na kitaifa ambazo mara nyingi zinaenea hadi nje ya mipaka yake. Kukiuka kanuni hizi kunaweza kuwa na madhara makubwa kwa wafanyakazi, kampuni au Kundi la Kampuni.

Pia wanazingatia nyaraka zinazotambulika kimataifa, kama vile zile zilizoandikwa na Umoja wa Mataifa. Limagrain lazima ifuate sheria hizi, na kusaini Ubunifu wa Kimataifa inaonyesha inadhamiria kuwa yenye nguvu kubwa na kuwa mfano katika eneo hili.

Matendo ya Limagrain ni jumla ya matendo mtu mmoja yanayofanywa na wafanyakazi wake, bila kujali nafasi zao au nchi wanayofanyia kazi. Kwa matendo yao ya kutii Kanuni za Nidhamu na Kanuni za Maadili Mema, jarida la ndani la Limagrain linalotumika linaelezea tabia ambayo Limagrain inatarajia kutoka kwa wafanyakazi wake, na mara nyingi Limagrain inakataza jambo kufanyika kwa niaba yake.

Wajibu wa Limagrain na watendaji wakuu, sifa na taswira yake nzuri zote ziko hatarini, lakini pia watendaji wakuu wanaamini jukumu la kijamii la kampuni ni lipi.

Hivyo, ni wazi kwamba kila mmoja anapaswa kutii Kanuni za Uadilifu na Kanuni za Maadili Mema, na kanuni zilizoelezwa kwenye jarida la ndani linalotumika!

## Je, kuna madhara gani kwa wafanyakazi katika kampuni yao?

Kukiuka Kanuni za Uadilifu na Kanuni za Maadili Mema kunawaweka wafanyakazi kwenye vikwazo vya kinidhamu vilivyowekwa kwenye hati inayosimamia kila kampuni kwenye Kundi (mara nyingi udhibiti wa ndani), na mwishowe kunaweza kusababisha mfanyakazi afukuzwe.

## Je, kuna madhara gani ya kisheria katika suala la rushwa?

Hasa hasa, kuhusu rushwa, kutofuata sheria inayohusiana na rushwa kunaweza kusababisha vikwazo vikubwa, mbali na vile ambavyo vinaweza kuwekwa na kampuni. Hakika, sheria ya kuzuia rushwa, kama vile sheria ya Sapin II nchini Ufaransa, vilevile masharti mengine mawanda ya kimataifa (Uingereza, Marekani, n.k.), inatoa adhabu za madai na jinai kwa wafanyakazi vilevile waajiri wao. Adhabu hizi zinatumika kwa wakosaji na washirika wake, bila kujali ikiwa wao ni watu au vyombo halali. Na mfanyakazi bado anawajibika hata kama amehusika katika tendo la rushwa kwa niaba ya na kwa manufaa ya kampuni yake. Mwisho, haijalishi kama rushwa ilifanikiwa au la; kusudio tu linawakilisha uhalifu ambao unaweza kupewa adhabu.



- **Kwa mfanyakazi**, kwa kuwa ni mtu, anaweza kuwajibishwa kwa adhabu, na adhabu inaweza kuwa miaka kadhaa jela, kupoteza haki za kiraia, na kukatazwa kufanya biashara husika, na inaweza kuhusisha faini kubwa sana.
- **Kwa upande wa Limagrain au kampuni zake tanzu**, pia linaweza kuwajibishwa. Hata kama hukumu zilizopendekezwa zinatofautiana kutoka nchi na ukanda mmoja hadi mwingine, karibia mifumo yote ya sheria inatoa hukumu za kwenda jela watendaji wakuu na faini ya jinai au uongozi kwa ajili ya kampuni. Faini hizi zinaweza kuwa kali sana na zinaweza kufika 30% ya mauzo ya kampuni, au zaidi. Wajibu wa kiraia wa kampuni unaweza pia kuhusishwa na kusababisha kiasi kikubwa cha fedha kuwalipa watu wengine ambao wamebainika kama waathirika wa tendo la rushwa.

## Adhabu nyingine zinazoweza kutolewa

- Kukatazwa kufanya shughuli fulani

Kukatazwa kushika madaraka yoyote ya umma au shughuli za kitaalam iliyohusishwa na kitendo cha rushwa linaweza kutangazwa. Kampuni iliyokutwa na hatia ya rushwa inaweza kukatazwa kushiriki katika miradi ya sekta ya umma. Katika Umoja wa Ulaya, kampuni iliyokutwa na hatia ya rushwa moja kwa moja inaondolewa kushiriki katika mikataba ya sekta ya umma. Mabenki yamekusanya orodha chafu ya kampuni zilizojihusisha na kesi za rushwa.

- Kutengwa katika baadhi ya wito wa tenda na miradi ya sekta binafsi

Kampuni za sekta binafsi mara nyingi zinakataa kufanya biashara na kampuni zinazotuhumiwa kwa ufisadi au ambazo zimekutwa na hatia ya ufisadi.

- Kufuta mikataba iliyopo

Mikataba iliyopatikana kwa ufisadi mara nyingi huchukuliwa kama batili kwa sababu ni ya udanganyifu.

- Sifa iliyoharibika

Kampuni zinazojulikana kujihusisha na ufisadi hasa hasa hutengwa katika masoko muhimu ya fedha na miamala ya kimataifa.

# FAHARASA

## RUSHWA:*

Rushwa bila shaka ni aina ya ufisadi inayofahamika zaidi. Pia ndiyo shabaha kuu ya sheria nyingi za kuzuia ufisadi. Kwa kawaida, rushwa ni kiasi cha fedha au zawadi iliyotolewa ili kupata manufaa yasiyo ya haki, yasiyostahili, au yasiyofaa.

Rushwa inaweza kuhusisha pande nyingi kwenye muamala, lakini kwa kawaida huhusisha angalau pande mbili: mtu anayelipa rushwa (mlipaji) na mtu anayepokea rushwa (mwombaji).

Rushwa si lazima iwe kiasi cha fedha; inaweza kuwa motisha ya fedha, huduma iliyotolewa au upendeleo, kwa mfano, ofa ya kumwajiri ndugu wa mtu ambaye anapokea rushwa. Hata ahadi ndogo ya kutoa kitu fulani hapo baadae kwa kubadilishana na maslahi ya kibiashara inawakilisha rushwa.

Rushwa inahusu masuala na vikundi vidogo mbalimbali kama vile:

- Hongo: aina ya rushwa, lakini ambayo inalipwa baada ya mkataba kutolewa, sio kabla. Kwa mfano, mtoa huduma binafsi ambaye anatarajia kupata ahadi ya mkataba analipa “hongo” kwa afisa wa serikali mara baada ya kupewa mkataba.
- Malipo ya uwezeshaji: malipo ya uwezeshaji, pia yanaitwa uwezeshaji, kulainisha kiganja cha mtu, kutoza kwa nguvu, au kulipa chini ya meza, ni kiasi kidogo cha fedha kinacholipwa moja kwa moja au visivyo moja kwa moja “kwa siri”, kwa afisa mwakilishi wa serikali, ili kuweka hakikisho au kuongeza kasi ya utendaji wa shughuli za kawaida au bila umakini, kama vile kupata viza, oda, au kuunganishwa kwenye mtandao (digitali, ya umeme, maji) kuharakisha hati ya utakaso wa ushuru wa bidhaa.
- Ushuru haramu: hii inamaanisha kodi au ada ya huduma ambayo ni haramu iliyotozwa na afisa ambaye hana mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

## KAZI ZA WATOTO:

Hii ina maanisha aina yoyote ya shughuli ya kiuchumi inayofanywa na watoto ambayo inaathiri maendeleo yao ya kimaadili, kimwili na kisaikolojia.

## NJAMA:

Njama ni makubaliano haramu, hasa yale ya siri, kati ya watu wawili au zaidi ili kumdhuru mtu mwingine kwa kumlaghai haki zake au kupotosha utaratibu. Hii inaweza kujumuisha, kwa mfano, usambazaji wa taarifa za siri kwenye soko na mtu ambaye anataka kutoa kipaumbele kwa mtoa huduma ili kumuwezesha kupata soko hilo; au uhamisho wa wafanyakazi ili kuficha mipango ya jamii.

## KAZI YA KUJIFICHA:

Hii inahusisha mtu ambaye anafanyakazi kwenye kampuni bila kuziarifu rasmi mamlaka husika.

## MGONGANO WA MASLAHI:*

*(angalia karatasi maalum ya taarifa za kiutendaji)*

Kwa mtu anayefanya shughuli za kitaalam (umma au binafsi), anashikilia ofisi iliyochaguliwa, au kutumia utumishi wa umma, mgongano wa maslahi unatafsiriwa kama kujiweka mwenyewe katika hali ambayo inaweza kuongeza mashaka kuhusu ushawishi wa kweli wa maamuzi ya mtu. Maslahi haya yanaweza kuwa ya ushirikiano, misaada, kitamaduni, kifedha, kisiasa, kidini, kimichezo, au matokeo ya ushirikiano wa kifamilia au kimapenzi.

Kwenye kampuni, ni hatari kwamba maslahi ya binafsi ya mfanyakazi yanaingilia maslahi ya kampuni; katika hali kama hiyo, huenda mfanyakazi hafuati tena masharti yake ya uaminifu kwenye kampuni.

Mgongano wa maslahi pia unaweza kujumuisha:

- uhusiano wa upendeleo (kifamilia au kifedha) na wateja, mkandarasi mwenza, au mkandarasi mdogo,
- kutumia ofisi ya kisiasa au kitaalam,
- kujilimbikizia shughuli za kitaalam,
- ndugu au jamaa wa karibu anapoomba nafasi ya kazi kwenye kampuni,
- kutumia au kugawa taarifa za siri kwa maslahi binafsi.

*(*) inarejelea jarida la ndani linalotumika.*

## UFISADI:

Ufisadi unajumuisha:

- zawadi, ahadi, au zawadi ya *manufaa yasiyo ya haki* mtu wa serikali au binafsi (ufisadi hai), au
- ushawishi, maombi, au kupokea manufaa *yasiyo ya haki* kutoka kwa mtu wa serikali au binafsi (ufisadi usio hai), ili kutimiza au kutotimiza jambo ikiwa ni sehemu ya kazi zake za kitaalam.

Tafsiri hii inadokeza kwamba:

- zawadi au ahadi inaweza kutolewa moja kwa moja au isiyo moja kwa moja, kwa mfano, kwa kupitia mtu wa kati;
- kile kinachotolewa kinaweza kuwa fedha taslimu au fadhila, kwa mfano, zawadi, mwaliko, au huduma fulani;
- kinachotarajiwa badala yake ni uteketezaji au

kutotekeleza.

## UBAGUZI:

Hii inahusu kukosekana kwa usawa katika ushughuli-kiaji watu kulingana angalau moja ya vigezo kama vile asili, jinsia, ulemavu, rangi ya ngozi, dini, n.k.

## KIKWAZO:

Kikwazo ni hatua ambayo inakataza ama miamala na nchi husika au miamala inayohusisha bidhaa lengwa na nchi husika; hii inadokeza kujua sababu za kiuchumi za muamala huo (m.f. katazo la kuuza silaha kwenye nchi X). Hatua za vikwazo zinazingatia maamuzi ya Umoja wa Mataifa au Umoja wa Ulaya au kanuni za nchi.

## UNYANG'ANYI:

Unyang'anyi unahusu kupata fedha, mali,

au huduma kutoka kwa mtu kwa ulghai au vitisho. Mara nyingi sana unahusu kufanya vitisho kumshawishi au kumlazimisha mtu mwingine kushughulikia au kufanya kitu fulani bila ridhaa yake, na hasa husababisha muathirika kupoteza fedha au kukubali faida fulani.

Katika mazingira ya rushwa, unaweza kuwahusisha watumishi au viongozi wa umma wanaotaka kupata kiasi fulani cha fedha, kwa vitisho kwamba vinginevyo atatumia ushawishi wake kuharibu kampuni au kumdhuru mtu. Mfano ni wakala wa forodha au ulinzi ambao wanakataa kufanya "uchunguzi" wa muda mrefu na wa gharama wa bidhaa flani au begi kwa kubadilishana na *rushwa*.

## WANAFAMILIA:

Hii inajumuisha ndugu, wa damu au wa kuoa/kuolewa (au mahusiano sawa na hayo yasiyo rasmi, ikiwemo mwenza, mpenzi, wazazi, au watoto. Ni pamoja na mtoto wa wazazi sawa, kwa kuoa/kuolewa au kuasiri, wazazi wa kambo, babu/bibi, wajomba, shangazi na binamu, wajukuu au ndugu yeyote ambaye anaishi kwenye kaya yako.

## MASLAHI YA FEDHA:

Neno "maslahi ya fedha" ni pamoja na, lakini sio tu, hisa yoyote au umiliki wa hisa, uwekezaji, mkopo uliotolewa au uliopokelewa, au makubaliano mengine ya fedha yaliyoingiwa mdau mwingine.

## KAZI YA LAZIMA:

Hii ni kazi inayofanywa kwa vitisho.

## UDANGANYIFU:

Udanganyifu unahusu kumdanganya mtu mwingine kwa makusudi ili kupata manufaa yasiyo ya kisheria au yasiyo halali au kukwepesha masharti ya kisheria, ya kawaida au ya mkataba.

Tabia ya udanganyifu inaonyesha tukio lilikusudiwa (sio kosa au kukosa umakini) ikiambatana na mchakato wa kuficha tendo lisiloidhinishwa.
Nia ya udanganyifu inaweza kuwa tofauti sana, na unaweza kutendwa kwa sababu ya fedha, uadilifu, au vitu. Kampuni inaweza kuwa muathirika au mnufaika wa udanganyifu.
Hivyo unaweza kuwa:

- matumizi mabaya ya fedha, vifaa, au taarifa za siri, au hata kutokuwa na uaminifu katika ubora wa bidhaa au huduma. Mifano inajumuisha kwa uongo unadai kuwa na nembo fulani au kufuata viwango fulani,
- kuharibu nakala za ushahidi,
- kudanganya maingizo ya mahesabu,
- kubandika sahihi iliyoskaniwa bila idhini ya wadau wengine,
- kushindwa kuujulisha umma au mtu binafsi, au azimio lenye makosa,
- kupotosha ukweli kwenye nakala ya mkataba, mahesabu, au utawala kama vile kutofuata viwango au vikwazo vinavyotakiwa na sheria.

## MAAZIMIO YA UDANGANYIFU:

Maazimio ya udanganyifu yanajumuisha makosa au urukaji wa makusudi wa taarifa ya kifedha, vilevile usambazaji wa taarifa ya kifedha kwa lengo la kutumia fursa ya wapokeaji, hasa wawekezaji na wadaiwa. Hii inaweza kumaanisha, kwa mfano, udanganyifu au urekebishaji wa faili za mahesabu na kifedha, kutofuata kanuni za mahesabu kwa makusudi, uwasilishaji wa uongo wa miamala, uondoaji au utoaji wa taarifa wa makusudi n.k.

Nje ya uwanja wa fedha, maazimio ya udanganyifu yanamaanisha makosa au uondoaji wa taarifa kwa hiari (Rasilimali Watu, kibiashara, n.k) katika nyaraka ya umma, kwa lengo la kumdanganya mpokeaji.

## KUTAIFISHA MALI:

Kuzuia mali za mtu kulikoamuliwa na mamlaka ya serikali (OFAC, Wizara ya Mambo ya Uchumi n.k.), kwa mujibu wa masharti ya nchi, kati ya nchi na nchi au vinginevyo, au kimataifa (UN) au Umoja wa Ulaya.

Uamuzi huu unahusu benki yoyote inayoshikilia mali kwa jina la mtu huyu na unashughulikia mali yote au sehemu ya mali kadri itakavyokuwa.

## ZAWADI*

Zawadi au ukarimu vinaweza kuwa vya namna tofauti kama vile bidhaa, chakula, safari, kukaa hotelini, mialiko ya matukio ya kitaalam, kitamaduni, au michezo au burudani nyingine.

## BAHASHISHI ISIYO HALALI:

Bahashishi sio halali ikiwa inatolewa kwa kutambua huduma iliyotolewa (uamuzi au kutoamua). Inaweza kuwa punguzo la bei la jumla ya fedha au zawadi ya thamani fulani. Ni namna ya ufisadi. Hili sio punguzo la bei ili kushawishi maamuzi au kutoamua kabla hakujafanyika, lakini punguzo la bei lililotolewa moja kwa moja kwa sababu ya maamuzi au kutoamua baada ya kufanyika.

(*) inarejelea jarida la ndani linalotumika..

## BIASHARA YA MWENYEJI:

Hii inahusu kutoa au kutumia taarifa ya "upendeleo" kwenye soko la hisa (hasa kwa kununua, kuuza, kubadilishana, kujisajili au kutumia machanuo), yaani taarifa mahususi na za siri ambazo zikiwekwa hadharani, zinaweza kuwa na athari hasa kwenye bei ya hisa.

Matendo kama hayo ni kosa linalomuweka mkosaji (wakosaji) kwenye mashtaka ya jinai. Ukiukaji huu pia unadhibitiwa na kuwekewa vikwazo na mamlaka za udhibiti wa soko la hisa ambalo hisa za kampuni zimeorodheshwa.

## KUSHAWISHI WABUNGE AU UWAKILISHI WA MASLAHI:

Huu ni mchango mzuri na wenye uwazi wa kampuni kwenye maendeleo ya kanuni au sera za umma kwenye jambo lenye maslahi kwake. Mchango huu unalenga kutoa taarifa ya mazingatio ya wafanya maamuzi ya umma.

## MATUMIZI MABAYA YA MALI NA FEDHA:

Neno hili linamaanisha wizi au matumizi ya udanganyifu ya mali ya kampuni na mtendaji mkuu au mfanyakazi. Matumizi haya mabaya yanaweza kuhusisha aina yoyote ya mali, ikiwemo rasilimali fedha, bidhaa, au aina nyingine zozote (zinazopoke-leka, vifaa vya kompyuta, au data zinazohusiana na taasisi ya kampuni au washirika wa kibiashara, kama vile marejeo ya mteja, taarifa za kiufundi kuhusu bidhaa au huduma, au taarifa nyingine za siri.

## MATUMIZI MABAYA YA MALI ZA KAMPUNI:

Hii inahusisha matumizi ya makusudi na binafsi ya mali za kampuni au mkopo au mamlaka aliyonayo afisa wa kampuni.

## UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU AU MTAJI:

Utakatishaji wa fedha haramu au mtaji inahusisha kuzipa muonekano halali bidhaa au fedha ambazo, kwa uhalisia, vimepatikana kwa njia haramu (ugaidi, biashara ya dawa za kulevya, kughushi, kudukua, ufisadi, ukwepaji kodi, n.k.) kwa kuficha asili yake. Pia unahusisha usafirishaji haramu wa fedha ili kuepuka udhibiti ya kubadilisha fedha na/au ugunduzi

wa mamlaka za kodi za mahali husika.

Unaweza kuwa wa namna zifuatazo:

- muamala ambao jina na taarifa za wahusika hazijulikani;
- muamala uliofanywa na walanguzi wasiojulikana au wasiofaa;
- muamala usio na maelezo;
- matumizi ya njia za malipo zisizo za kawaida;
- muamala kutoka nchi tofauti na ile ambayo huduma imetolewa au tofauti na kule ambako ofisi kuu ilipo.

## UPENDELEO:

Hii inahusisha *kutoa manufaa* yasiyo ya haki kwa wanafamilia, marafiki na ndugu zake.

## DATA BINAFSI:

Hii inamaanisha data ambazo zinamtambulisha mtu binafsi moja kwa moja au visivyo moja kwa moja kama vile jina la ukoo, jina la kwanza, namba ya simu, barua pepe, n.k.

## MASLAHI BINAFSI:

Neno "maslahi binafsi" linatakiwa lieleweke kwa mawanda mapana, yaani, kuhusisha maslahi ya mtu husika (mwajiriwa, mfanyakazi, kiongozi wa umma, mjumbe wa uongozi, utumishi wa umma, au serikali) na ya wale wa familia yake au ndugu wake wa karibu (ndugu wa asili au kisheria).

## WATU WALIOJIINGIZA KWENYE SIASA (PEP):

Hawa ni watu ambao wanamiliki au wamemiliki nafasi ya uaminifu na mamlaka katika ngazi ya juu ya utumishi wa umma, au kazi za kisiasa, kisheria, kiutawala , au kazi ndani ya taasisi ya kimataifa, vilevile mwanafamilia wa karibu au ndugu wa karibu. Hasa, watu hawa wanahudumu katika ofisi kubwa za kisiasa, kama vile viongozi wa serikali, wanasiasa wenye hadhi ya juu au viongozi wa umma wenye hadhi ya juu, mahakimu au maafisa wa jensi wenye vyeo vya juu, vilevile kama watendaji wakuu wa kampuni za umma au vyama muhimu vya siasa.

## AFISA WA SERIKALI AU MWAKILISHI WA SERIKALI:

Viongozi wa umma au mwakilishi wa serikali inamaanisha:

- kiongozi yeyote wa umma ambaye amechaguliwa au ameteuliwa kama mjumbe wa wizara, au kama mbunge,
- mfanyakazi yeyote au mtu anayefanyakazi kwa ajili ya au kwa niaba ya, kiongozi wa umma, shirika la serikali, au kampuni inayofanya kazi kwa ajili ya, au inayomilikiwa au inayosimamiwa na shirika la serikali, kama vile mtafiti aliyeajiriwa na chuo cha serikali,
- afisa yeyote wa chama cha siasa, mteuliwa mwenye mamlaka mteuliwa, afisa au mfanyakazi au mtu anayefanya kazi kwa ajili ya, au kwa niaba ya, chama cha siasa au mteuliwa mwenye mamlaka rasmi,
- mfanyakazi au mtu yeyote anayefanya kazi kwa ajili ya, au kwa niaba ya, shirika la umma la kimataifa,
- mshirika yeyote wa familia ya kifalme au jeshi,
- mshirika yeyote wa "Serikali", neno linalorejelea ngazi zote na vitengo vidogo vya serikali (serikali ya mtaa, mkoa, au taifa, na utawala, bunge, au serikali).

Ndugu wa karibu wa watu hawa wote pia wanachukuliwa kama viongozi wa umma.

## WADAU:

Mdau ni mtu yeyote anayetambulika kisheria au kiuadilfu, au kundu la watu au taasisi ambayo inaweza kuhusishwa, moja kwa moja au visivyo moja kwa moja, na shughuli ya wabia, kampuni, au kundi la kampuni. Hii inashughulikia wahusika wakuu kama vile: wawekezaji, wafanyakazi, waajiriwa, wasambazaji, wakandarasi wadogo, wateja, mamlaka za umma, taasisi za kitaalam, vilevile taasisi za kimataifa, NGO, jumuiya za mahali husika, waandishi wa habari na vyombo vya habari.

## KAMPUNI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI (KAMPUNI ZA UMMA):

Kampuni za umma ni vyombo halali ambavyo vinamilikiwa na serikali kwa ujumla wake au sehemu, au vilivyo chini ya usimamizi wa serikali. Wafanyakazi na wawakilishi wa kampuni zinazomilikiwa na serikali wanachukuliwa kama wawakilishi wa serikali au *viongozi wa umma* kwa mujibu wa sheria za kuzuia ufisadi.

## MANUFAA YASIYO YA HAKI AU YASIYOHALALISHWA:

Manufaa yasiyo ya haki yanafafanuliwa kama kitu au huduma ya thamani iliyotolewa kwa mnufaika kwa dhumuni la kupata uamuzi au kutopiga kura, au kuathiri uamuzi. Mnufaika anaweza kuwa kiongozi wa umma, mfanyakazi kutoka sekta binafsi, ndugu wa mtu huyo (mwanafamilia) au chombo kinachohusiana (wakfu, kampuni ya mafuta, n.k.).

Manufaa haya isiyo ya haki yanaweza kuwa:

- moja kwa moja (kwa mfano, malipo chini ya meza, ada zisizo sahihi au kupunguza asilimia ya faida, malipo ya uwezeshaji au fedha taslimu, huduma, punguzo la bei, zawadi za kifahari au faida nyingi, malipo makubwa ya huduma, deni, mkopo),
- au isiyo ya moja kwa moja (kwa mfano, malipo kwenda chama cha siasa, misaada na ufadhili, zawadi ya nafasi au mafunzo kwa vitendo, n.k.

# ANDIKA

## **Rushwa:** aina ya ufisadi inayojulikana zaidi inajitokeza katika namna nyingi duniani kote

### *Misri*


- *Ashaan ad-dukhaan (kitu chochote kwa ajili ya sigara zako)*
- *Ashaan ash-shay (kitu chochote kwa ajili ya chai yako)*
- *Bakchich (zawadi, rushwa, mchango)*
- *Barteel rashwah (rushwa)*
- *Kahwa (kahawa)*

### *Urusi*

- *Vzyatka (rushwa)*
- *Dat' na lapu (grisi)*

### *China*

- *Chaqian (hela ya chai)*
- *Zou hou mien (njoo kinyume nyume)*



### *Marekani*

- *Rushwa*
- *Hongo*
- *Payola*
- *Kitia utam/Hongo*
- *Hela ya hongo*
- *Grisi*
- *Lowesha mdomo wangu*

### *Meksiko*

- *Soborno (rushwa)*
- *Mordida (kitafunwa)*
- *Refresco (kinywaji)*
- *Dinero por debajo de la mesa (grisi)*

### *Peru*

- *Coima (msimu ya rushwa)*

### *Irak*

- *Kahwa (kahawa nzuri)*

### *Nigeria*

- *Kola, dash, egunje (rushwa)*

### *Angola*

- *Gaseoso (kinywaji)*

### *Romania*

- *Rasplata (zawadi kwa ajili ya huduma)*

### *Thailand*

- *Sin bone (hela ya chai)*

### *India*

- *Rishwat (grisi)*
- *Baksheesh; ghoos, hafta (rushwa)*
- *Chai-pani (chai na maji)*

### *Uturuki*

- *Rusvet (rushwa)*

### *Ufilipino*

- *Lagay (nipe tano)*
- *Kotong, suhol (rushwa)*

Limagrain
*from earth to life*

Kanuni hizi za Uadilifu na Kanuni za Maadili Mema ni sehemu ya maeneo ya maandiko mbalimbali ya kimataifa ambayo Limagrain inazitumia kanuni hizo:

- Azimio la Haki za Binadamu;
- mikataba ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani, hasa mikataba namba 29, 105, 138 na 182 (kazi ya mtoto na kazi ya shuruti), 155 (afya na usalama wa wafanyakazi), 111 (kuzuia ubaguzi), 100 (ujira), 87 na 98 (uhuru wa kushirikiana, haki ya kuanzisha chama cha wafanyakazi ili kujadiliana pamoja);
- Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto;
- miongozo ya OECD kwa ajili ya kampuni za kimataifa;
- Kanuni za Ubunifu wa Duniani katika Umoja wa Mataifa, zilizotiwa sahihi na Limagrain mnamo Desemba 2013.
- sheria ya Ufaransa inayoitwa “Sapin II” inayotumika kuanzia Juni 1, 2017;
- mabadiliko kwenye sheria ya Ufaransa ya Agizo la Ulaya la Oktoba 22, 2014, linaloitwa “CSR”.

All Contents – RCS 495 289 399 – RCS 352 321 285 - 22020050 - 05/2022